

**TAARIFA YA KATIBU MKUU OFISI YA RAIS IKULU, BW. MULULI
MAHENDEKA, KWA KATIBU MKUU KIONGOZI MHE. BALOZI DKT. MOSES
MPOGOLE KUSILUKA, WAKATI WA UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA 6
CHA SERIKALI MTANDAO KATIKA UKUMBI WA
AICC – JIJINI ARUSHA, FEBRUARI 17, 2025**

Mhe. Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka; Katibu Mkuu Kiongozi

Makatibu Wakuu wote,

Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya,

Dkt. Musa Kissaka; Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),

Mhandisi. Benedict Ndomba; Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),

Wakuu wa Taasisi za Umma na Binafsi,

Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali

Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao;

Viongozi wa Dini,

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana;

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;

Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema, na kutuwezesha kukutana hapa leo katika Kikao Kazi hiki cha Sita (6) cha Serikali Mtandao.

Napenda kukushukuru wewe **Mhe. Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi**, kwa kutenga muda wako na kuwa nasi katika ufunguzi wa kikao hiki muhimu. Tunatambua majukumu yako mazito ya kitaifa, na uwepo wako hapa unaonesha dhamira ya dhati ya Serikali katika kuimarisha ajenda ya Serikali Mtandao. Tunakukaribisha sana.

Aidha, napenda kuwashukuru viongozi wote wa Serikali, Wakuu wa Taasisi za Umma na Binafsi, Watumishi wa Serikali, Sekta Binafsi, viongozi wa dini, pamoja na Waandishi wa Habari kwa kushiriki kikao hiki kinacholenga kuimarisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

Vilevile, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mwenyeji wetu, **Dkt. Toba Alnason Nguvila Katibu Tawala Mkoa wa Arusha**, kwa kutupokea vyema na kuhakikisha usalama na mazingira rafiki kwa ajili ya kufanyika kwa kikao hiki.

Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;

Katika kipindi hiki cha mabadiliko ya kasi ya teknolojia, Serikali Mtandao imeendelea kuwa nyenzo muhimu katika kuimarisha utawala bora na ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kwa kutambua hilo, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), na kuipa jukumu la kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao, pamoja na kuhakikisha uzingatiaji wa sera, sheria, kanuni, miongoza na viwango vya serikali mtandao katika taasisi za umma.

Lengo ni kujenga Serikali Mtandao kwa kutumia teknolojia za kisasa kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii, huku tukihakikisha mifumo ya TEHAMA inakuwa salama, inasimamiwa ipasavyo na inalinda maslahi ya Taifa.

Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;

Kikao Kazi hiki cha Sita kinawakutanisha wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao, ambao watajadili hali ya utekelezaji wa jitihada hizi, ikiwemo kusimamia matumizi sahihi ya teknolojia zinazoibukia, kama Akili Mnemba na nyinginezo, katika kuboresha utendaji kazi wa Serikali na utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, kikao hiki kinatarajiwa kutoa maazimio ya pamoja yatakayosaidia kuimarisha utekelezaji wa ajenda ya Serikali Mtandao, na Serikali itahakikisha maazimio hayo yanasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo kupitia e-GA.

Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;

Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, itaendelea kuimarisha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa kuitengea rasilimali, pamoja na kuimarisha miundombinu ya TEHAMA kulingana na mahitaji na mabadiliko ya teknolojia.

Aidha, mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, yameiwezesha Tanzania kutambuliwa kimataifa, ikiwemo kutajwa na Benki ya Dunia katika eneo la ukomavu wa matumizi ya TEHAMA Serikalini kwa mwaka 2025.

Serikali inaridhishwa na mchango wa e-GA katika kuleta mageuzi ya matumizi ya TEHAMA kwenye taasisi za umma na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu.

Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;

Nikuhakikishie kuwa, ofisi yangu itaendelea kuisimamia e-GA na kuhakikisha maazimio yote yatakayotolewa hapa yanatekelezwa.

Nihitimishe kwa kukushukuru tena wewe **Mhe.. Katibu Mkuu Kiongozi**, pamoja na washiriki wote wa kikao hiki. Ninawatakia kikao chema chenye mafanikio washiriki wote.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

“Kwa pamoja tujenge Serikali Mtandao.”